# Serikali yatoa tamko samaki waliokufa

Na Romana Mallya

SERIKALI imeruhusu shughuli za uvuvi kuendelea katika Soko la Kimataifa la Samaki Feri wakati uchunguzi ukiendelea kuhusu samaki waliokutwa wamekufa katika ufukwe uliopo karibu na Hospitali ya Aga Khan na Ocean Road jijini Dar es Salaam.

Jana, Nipashe iliandika habari kuhusiana na samaki hao waliokutwa juzi ufukweni wakiwa wamekufa.

Taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, iliwatoa hofu wananchi na kuwataka waendelee na biashara ya samaki katika soko hilo.

'Wizara hiyo iliahidi kutoa taarifa ya uchunguzi wa vifo vya samaki hao mara baada ya kukamilika kwake na kubainisha kuwa walishateketezwa.

"Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi inapenda kuwashukuru wananchi wote waliokuwapo kwenye ufukwe wa Hospitali ya Aga Khan na Ocean Road pamoja na Soko la Magogoni Feri wakati wa tukio hili kwa ushirikiano mkubwa walioounyesha uliofanikisha kuzuia kuingizwa kwa samaki hawa sokoni na hatimaye kuteketezwa na Ofisa Uvuvi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam," ilibainisha.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa sampuli za samaki hao zilichukuliwa kwa ajili ya maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), Maabara ya Taifa ya Uvuvi (Dar es Salaam) na Jeshi la Polisi Kitengo cha Sayansi ya Uchunguzi kwa ajili ya kupeleka Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Pia taarifa hiyo ilisema baada ya kuimarisha ulinzi eneo la Soko la Magogoni na eneo la tukio, wananchi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, maofisa wa wizara, TAFIRI, maofisa uvuvi wa Halmashauri ya Jiji wakiwa na mameneja wa Soko la Feri, walikusanya kiasi cha kilo 164 na kukifikisha Kituo Kikuu cha Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

Scanned with CamScanner

HABARI LEO UK 8.

# Samaki waliokufa ufukweni wateketezwa

Na Mwandishi Wetu

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema maofisa uvuvi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na na vyombo mbalimbali vya serikali vimefanikiwa kuzuia kuingia sokoni kwa samaki waliokufa baharini na wameweteketeza.

Aidha, imesema jumla ya kilo 164 za samaki waliokufa na kuelea ufukweni jirani na Hospitali ya Aga Khan na Ocean Road mkoani Dar es Salaam, zimechukuliwa na kupelekwa maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuchunguzwa sababu ya vifo vyao na majibu yakitoka umma utajulishwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na wizara hiyo, ofisi ndogo ya wizara hiyo Dar es Salaam, ilipokea taarifa kutoka Polisi Ilala za kuelea kwa samaki waliokufa katika ufukwe huo.

Ilisema baada ya taarifa hizo maofisa uvuvi wa Halmashauri ya Jiji kwa kushirikiana na wananchi na mamlaka mbalimbali za serikali walifanikiwa kuwakusanya samaki hao na kudhibiti wasiingie katika soko na baada ya kuchukuliwa sampuli, kilo 156 zilizobaki kati ya 164 ziliteketezwa.

Uteketezaji huo uliwafanywa na maofisa uvuvi wa halmashauri hiyo na kushuhudiwa na maofisa wa wizara, uongozi wa Soko la Feri, Ofisi ya Uvuvi Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na wananchi waliokuwepo Soko la Magogoni Feri.

"Tunawashukuru wananchi na mamlaka zote za serikali waliofanikisha kudhibiti samaki hao, sampuli zimeshachukuliwa na kupelekwa maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kubaini chanzo cha vifo vyao na majibu yakitoka, umma utajulishwa," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Hata hivyo, sampuli hizo zilichukuliwa pia na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) kwa ajili ya maabara yao, maabara ya Taifa ya Uvuvi (Dar es Salaam).

Wizara iliwashukuru wananchi wote waliokuwepo kwenye ufukwe wa hospitali hizo pamoja na Soko la Magogoni Feri wakati wa tukio hilo na kutoa ushirikiano uliofanikisha kuzuia kuingizwa kwa samaki hao sokoni na kuteketezwa.

Aidha, imewataka wananchi kuendelea na biashara ya samaki katika Masoko ya mkoa wa Dar es Salaam kama ilivyo kawaida.

Juzi picha na video zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii zikionesha katika fukwe hizo samaki waliokufa wakielea majini na ndipo vyombo vya usalama wakiwepo polisi wakachukua hatua.

Mkurugenzi wa TAFIRI, Dk Ismail Kimerei alikiri kuwepo wa samaki hao katika eneo hilo na kusema mamlaka mbalimbali za serikali za usalama na ulinzi walifika wakiwemo wao na kuchukua sampuli ili kupelekwa maabara.

Scanned with CamScanner

NAIBU Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo Mathew (wa pili kulia) akitoa pole kwa wafiwa na waombolezaji waliokuwa katika msiba Kijiji cha Magila Gereza wilayani Korogwe alipotembelea kijijini hapo kukagua ubora na upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika eneo hilo. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Basilla Mwanukuzi. (Picha na Wizara ya Habari)

kuhakikisha tunakaa katika utaratibu ambao wataalamu wa afya wanatuelekeza ili kujikinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya Corona.

UHURU UK 19.

# Serikali yachunguza sababu vifo vya samaki

Dar es Salaam
NA IRENE MWASOMOLA

SIKU moja baada ya kuonekana samaki wanaoelea katika fukwe za Bahari ya Hindi eneo la Aga Khan jijini Dar es Salaam, serikali imesema baada ya uchunguzi kukamilika umma utajulishwa chanzo cha vifo hivyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ilisema baada ya kutokea tukio maofisa wa wizara kwa kushirikiana na polisi walifika eneo hilo kuchukua samaki hao ili kuzuia kuingizwa sokoni.

"Julai 21, mwaka huu saa tatu asubuhi, ofisi ndogo ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi jijini Dar es Salaam, ilipokea taarifa kutoka Polisi Mkoa wa kipolisi Ilala kuhusu tukio la kuelea samaki waliokufa katika ufukwe uliopo karibu na Hosptali ya Aga Khan," ilieleza.

Aidha taarifa hiyo ilisema Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFRI) kwa kushirikiana na Ofisa Uvuvi wa Jiji la Dar es Salaam na uongozi wa soko la feri waliteketeza samaki hao kilogramu 156.

Vilevile, taarifa hiyo ilieleza baada ya tukio hilo sampuli zilichukuliwa kwa ajili ya vipimo vya maabara ya TAFRI, Maabara ya Taifa ya Uvuvi na Polisi kitengo cha Sayansi ya Uchunguzi ili kupeleka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Juzi, saa nne asubuhi baadhi ya wananchi waliingiwa na taharuki kufuatia tukio la samaki kuoneka wamekufa katika eneo la fukwe karibu na Hospitali ya Aga Khan.

Wakizungumza na gazeti hili, mashuhuda na watu waliokuwa wanaokota samaki hao walisema ni mara ya kwanza katika eneo hilo kuonekana samaki wakiwa katika hali hiyo.

Mfanyabiashara wa madafu katika ufukwe huo, Shanibi Swalehe, alisema kabla ya samaki hao kuonekana uliibuka upepo wenye mawimbi makali na kusababisha maji kujaa tangu saa nne asubuhi.

"Tangu saa nne asubuhi samaki walikuwa wengi, mimi nimeokota wengi na wengine wamejaza viroba, lakini walifika askari na kutunyang'anya," alisema.

Naye, Mkazi wa Kigamboni, Shabani Hosen, alisema aliokota samaki zaidi ya kilo tano lakini polisi walifika eneo hilo kuwazuia wananchi wasiendelee kuokota samaki hao kwa ajili ya usalama wao.

Meneja wa Soko la Kimataifa la Samaki Feri, Denis Mrema, akikiri kutokea kwa tukio hilo na kueleza kwamba walishirikiana na polisi kuchukua sampuli kisha kupeleka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kubaini usalama wa samaki hao.

"Tumeteketeza baadhi ya samaki na sampuli zimechukuliwa ili kupelekwa kwa Mkemia Mkuu," alibainisha Mrema.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Muliro Jumanne, alipoulizwa na gazeti hili kuhusu taarifa hizo alisema, polisi wahahusiki na masuala hayo.

"Mimi na samaki wapi na wapi? Jeshi la Polisi na samaki wapi na wapi? Waulize watu wa uvuvi....mimi niulize masuala ya waharifu na majambazi,"alisema.

Scanned with CamScanner

maeneo maalumu ya vivuko kwa kufuata maelekezo ya alama zilizopo kuepuka ajali zinazoweza kuleta madhara," alisema.

# Watatu wafa mapigano wakulima na wafugaji

UHURU UK 2

Lindi
NA SOPHIA NYALUSI

WATU watatu wamefariki dunia na wengine zaidi ya 50 wanashikiliwa na polisi mkoani hapa kwa tuhuma za kushiriki mapigano baina ya wakulima na wafungaji yaliyotokea Kijiji cha Nanjilinji wilayani Kilwa, mkoani Lindi.

Mapigano hayo yalitokea juzi saa saba mchana baada ya mkulima, Chande Magoma, kumkamata mfugaji aliyekua akilisha mahindi katika shamba lake.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Mtatiro Kitinkwi, alisema mapigano hayo yalisababishwa baada ya kuibuka mgogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Katika tukio jingine, kamanda huyo alisema watu wanne wakazi wa Kijiji cha Namkongo, Kata ya Mipingo, Manispaa ya Lindi, wamekamatwa wakiwa na viroba 15 vya bangi vyenye uzito wa kilo 725 na mbegu kilo 942.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Lindi wanaofanya shughuli haramu kuacha mara moja kwa sababu mkoa huo una fursa mbalimbali kuwawezesha kuendesha maisha yao bila kuvunja sheria za nchi.

Scanned with CamScanner



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akizungumza katika mkutano wa hadhara na Wakazi wa Kijiji cha Mchinga Namba Mbili wilayani Mchinga mkoani Lindi wakati wa ziara yake ya kikazi ambako alibainisha kwamba wizara wataandaa mfumo shirikishi wa kupambana na uvuvi haramu siku zote, badala ya kuwa na operesheni za vipindi maalum.** (Picha zote za mtandaoni)

# Udhibiti wa uvuvi haramu na ongezeko mavuno ya samaki

"Katika bahari tulikamata meli moja ya uvuvi Mtwara ya kutoka Vietnam, na wahusika walifungwa."

Dkt Tamatamah anasema kuwa tangu mwaka jana, Wizara ya Mifugo na Uvuvi walianzisha mkakati shirikishi wa usimamizi wa udhibiti wa rasilimali za uvuvi wenye mamlaka za serikali za mitaa, ili kuimarisha ulinzi shirikishi.

"Baada ya kukamilika kwa ile operesheni, idadi ya samaki wenye maziwa, bahari na mito imeongezeka kwa kiasi kikubwa.

"Miaka ya nyuma kabla ya operesheni ile, mavuno ya samaki Tanzania kutoka vyanzo vyote vya maji yalikuwa tani 150,000 hadi 360,000.

"Lakini kwa mara ya kwanza mwaka 2019 zilifika tani 482,000, na mwaka jana ulifika tani 497,000," anasema.

Kuhusu idadi ya wavuvi waliopo nchini, anasema kuwa Tanzania ina wavuvi wanaotambulika 253,000, na kwamba waluga samaki ni 0,000.

Anabainisha kuwa, kesi zilizopo mahakamani kuhusu uvuvi haramu hazizidi 10, kwa sababu wengi hulipa faini.

Mbunge wa Chonga, Salum Shaafi (ACT Wazalendo) anasema kuwa, kuchoma nyavu za wavuvi si suluhisho dhidi ya uvuvi haramu, kwamba serikali inapaswa kuwapatia mikopo wavuvi, ili wanunue zana za kisasa za uvuvi, ikiwemo boti za uvuvi.

Mbunge huyo anasema kuwa pia serikali iendelee kutoa elimu kuhusu athari zinazosababishwa na uvuvi haramu.

"Uvuvi umetoa ajira kwa Watanzania, hivyo ni jukumu la serikali, hasa ni kutoa elimu, ili wananchi waondokane na uvuvi haramu unaoharibu mazalia ya samaki, unaoharibu utalii, kwa kuwa bahari na maziwa ni sehemu ya vivutio vya utalii," mbunge amesema.

## KUHUSU MIKOPO

Dkt Tamatamah, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), anasema kuwa mwaka 2018 lilianzishwa dawati la sekta binafsi, ili wavuvi waweze kukopesheka.

Anaendelea kusema kwamba, kabla ya mwaka 2018 ilikuwa hakuna mtu yeyote au kikundi chochote kilichopata mikopo benki, lakini kwamba mpaka Aprili, mwaka huu, kuna vikundi ambavyo vimepata mikopo kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

"Kwa mfano, Ukerewe kuna akinamama wanaofanya kazi ya kuanika dagaa, ambao ni tatizo kuanikwa wakati wa masika, tukawaunganisha na kusaidia kuwaandikia pendekezo na kulipeleka Benki ya TADB.

"Na walipata mkopo wa shilingi milioni 200, walizotumia kununua mashine kwa ajili ya kukausha samaki.

"Kikundi kingine kinaitwa Iragula kilichopo Sengerema, ambao walinunua boti za kuvulia na nyavu," anasema Dkt Tamatamah.

## WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI

Wakati akiwasilisha mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya wizara yake kwa ajili ya mwaka 2021/2022 siku za karibuni bungeni, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema kuwa katika mwaka 2020/2021 sekta ya uvuvi nchini ilikua kwa asilimia 6.7.

"Pia mchango wa sekta hii kwa pato la taifa ulikuwa asilimia 1.71, na kutoa ajira za moja kwa moja kwa wavuvi 195,435, wakuzaji viumbemaji 30,064, na Watanzania milioni 4.5 wameendelea kupata mahitaji yao ya kila siku, kutokana na shughuli mbalimbali zinazohusiana na sekta ya uvuvi," alisema waziri.

Ndaki alisema kuwa, shughuli za wavuvi wadogo huchangia asilimia 95 ya samaki wote wanaovuliwa nchini, na kwamba asilimia tano iliyobaki huchangiwa na wavuvi wakubwa.

Zaidi kwamba, hadi April, mwaka huu, wavuvi wadogo 195,435 walishiriki moja kwa moja shughuli za uvuvi kwa kutumia vyombo vya uvuvi 58,231, na kuwa walivuna tani 422,859.8 za samaki wenye thamani ya sh trilioni 2.62.

"Kulingana na taarifa za utafiti katika Ziwa Victoria mwaka 2020, kiasi cha samaki katika ziwa hilo kimeongezeka kutoka tani milioni 2.7 mwaka 2019 hadi tani milioni 3.5 kwa ziwa zima, ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 29.3.

"Ongezeko hili limechangia kiasi cha samaki kilichopo katika maji yote kufikia tani milioni 4.1," amesema Ndaki.

> *Kulingana na taarifa za utafiti katika Ziwa Victoria mwaka 2020, kiasi cha samaki katika ziwa hilo kimeongezeka kutoka tani milioni 2.7 mwaka 2019 hadi tani milioni 3.5 kwa ziwa zima, ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 29.3. Ongezeko hili limechangia kiasi cha samaki kilichopo katika maji yote kufikia tani milioni 4.1 ...*
>
> **Mashimba Ndaki**
> Waziri wa Mifugo na Uvuvi

Scanned with CamScanner



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt Rashid Tamatamah.**

# Udhibiti wa uvuvi haramu na ongezeko mavuno ya samaki

***Na Mwandishi Wetu***

CHIMBUKO la Siku ya Uvuvi Haramu Duniani ni wazo lililoibuliwa mwaka 2015 katika Kikao cha 39 cha Kamisheni ya Nchi za Mediterranean.

Kikao hicho kilipendekeza iwepo siku ya kimataifa ya kuhamasisha kudhibiti uvuvi haramu, ambao taarifa zake huwa hazitolewi na wala shughuli zake haziratibiwi.

Kamisheni hiyo walipendekeza siku hiyo itangazwe, ili kuwasilisha uelewa kuhusu umuhimu wa vita dhidi ya uvuvi haramu.

Pendekezo hilo liliwasilishwa na kuridhiwa katika Kikao cha 32 cha Kamati ya Uvuvi ya Shirika la Chakula Duniani (FAO).

Akizungumzia siku hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt Rashid Tamatamah, anasema kuwa Desemba 2017 Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika maazimio yake ya mwaka kuhusu uvuvi endelevu, walitangaza rasmi Juni 5 kila mwaka kuwa ni 'Siku ya Kimataifa ya Vita Dhidi ya Uvuvi Haramu, Uvuvi Usiotolewa Taarifa na Usioratibiwa'.

Dkt Tamatamah anasema kuwa, Juni 5 ilichaguliwa kwa sababu wakati azimio hilo linapitishwa, kulikuwa na itifaki ya kuzuia uvuvi haramu kupitia bandari.

Anasema kuwa Tanzania iliridhia itifaki hiyo iliyolenga kudhibiti uvuvi haramu, na kwamba siku ambayo itifaki hiyo ilipitishwa ilikuwa Juni 5, hivyo Umoja wa Mataifa (UN) waliona ni vyema tarehe hiyo iendelee kwa kuwa inahusu uvuvi haramu.

Anaendelea kusema kuwa, kwa sababu Tanzania ilishaidhia itifaki hiyo na kuunga mkono azimio la Umoja wa Mataifa dhidi ya uvuvi haramu, serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi wamedhibiti uvuvi haramu kwa asilimia 80 kwenye majibaridi (maziwa, mito na mabwawa).

Kadhalika, kwamba wamedhibiti uvuvi haramu kwa asilimia 100 kwenye majichumvi, hususan Bahari ya Hindi ambako kuna aina kubwa za uvuvi haramu uliokuwa ukifanyika, hasa wa kutumia milipuko ya baruti.

"Uvuvi haramu ni dhana pana ambayo pamoja na kuhusisha matumizi ya nyavu zisizoruhusiwa, pia inahusisha kitendo cha mtu kuvua bila kuwa na leseni, kutumia chombo cha uvuvi ambacho hakijasajiliwa, na utoroshaji wa samaki kwenda nje ya nchi," Dkt Tamatamah anasema.

Pamoja na serikali kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kudhibiti uvuvi haramu, Dkt Tamatamah anasema kuwa, changamoto za matumizi ya makokoro, watu kuvua bila leseni, na utoroshaji samaki kwenda nje ya nchi, bado zipo japo kwa kiasi kidogo.

"Kabla ya mwaka 2017, hali ilikuwa mbaya sana, lakini mwaka 2018, idara, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, waliendesha operesheni mwaka mzima, ikiwemo ***Operesheni Sangara*** katika Ziwa Victoria na ***Operesheni Jodari*** katika Bahari ya Hindi, zilizofanikiwa kuondoa nyavu haramu," anasema.

**INAENDELEA UK. 14**

Scanned with CamScanner